



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.CDC/A.10/17/73

01 Oktoba, 2021

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI MTENDAJI WA KIJJI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino anakaribisha maombi ya Kazi kutoka kwa Watanzania wenye Sifa na Uwezo wa Kujaza nafasi ya **Mtendaji wa Kijiji III**. Tangazo hili ni baada ya kupokea barua ya Kibali cha Ajira Mbadala chatarehe **10/09/2021** yenye Kumb.Na.FA.170/360/01/161 kutoka kwa Katibu Mkuu, OR – UTUMISHI.

### 1. MTENDAJI WA KIJJI III NAFASI SABA (07)

#### 1.0 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu Kidato cha IV au VI aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika mojawapo ya Fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### 1.1 MAJUKUMU

- i. Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kuondoa Njaa, Umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- viii. Kusimamia ukusanyaji na kuhifadhi kumbukumbu zote za Nyaraka za Kijiji.
- ix. Kupokea, kusikiliza, na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- x. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na

## 1.2 MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Serikali TGS. B

## 2. MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye Umri kati ya Miaka 18 hadi 45.
- ii. Mwombaji awasilishe Picha moja ya hivi karibuni (passport size).
- iii. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (referees) wa kuaminika.
- iv. Waombaji wote waambatanishe nakala ya Vyeti halisi vya Masomo na Taaluma masomo (NTA Level 5) na transcript ya cheti cha Taaluma, Cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha "Result Slip", "Statement of Results", "Provisional Results" au "Transcript" bila nakala halisi ya Cheti cha Taaluma maombi yake hayatakubaliwa.
- v. Kwa waliosoma Nje ya Nchi Elimu ya Kidato cha nne na Kidato cha Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- vi. Wote watakaochaguliwa kufanya usaili ndio watakaoitwa kwenye Usaili (Interview).
- vii. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa.
- viii. Maombi yaandikwe kwa Mkono na yatumwe kwa Njia ya Posta kupitia Anwani iliyotajwa hapo chini.
- ix. Awe ambaye hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- x. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe: 18/10/2021

**MUHIMU: KUMBUKA KUAMBATANISHA BARUA YAKO YA MAOMBI  
YA KAZI ILIYOSAINIWA PAMOJA NA VYETI VYA ELIMU.**

### MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino,  
S.L.P. 1126,  
**CHAMWINO – DODOMA.**

TANGAZO hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino:[www.chamwinodc.go.tz](http://www.chamwinodc.go.tz)



Dkt. Semistatus .H. Mashimba,  
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri,  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO  
S. L. P. 1126  
DODOMA**

---

S.L.P.1126, Chamwino - Dodoma, Simu(026)2961511 Nukushi: (026)2961511, Barua pepe:ded@chamwinodc.go.tz  
**TOVUTI:www.chamwinodc.go.tz**